

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**16 JUNI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI – TAREHE 16 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

430. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY  
MAGANGA (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza Barabara zote mbovu zilizopo katika Jimbo la Mbogwe.

431. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI  
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka uwiano sawa wa mikopo ya asilimia 10 inayotokana na

mapato ya ndani bila kujali mapato ya Halmashauri husika ili kusaidia wanufaika wa mikopo wanaoishi nje ya Miji wapate fursa sawa na wanufaika wa Mijini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**432. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

- Je, ni Taasisi ngapi zimeweza kujisajili na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi nchini (*Green Climate Fund*) hadi sasa na Miradi mingapi imeshaombewa Fedha kupitia Mfuko huo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**433. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, uwepo wa Kiwanda cha kuua mazalia ya Mbu (*Tanzania Biotech Product Limited*) umesaidia vipi mapambano dhidi ya Malaria nchini.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**434. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Igunga.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**435. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya kutoka Katumbasongwe hadi Ileje, Km. 90.7 itaanza kujengwa.

**436. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-



Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Tarime hadi Serengeti kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**437. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Mihimili muhimu ya uchumi wa soko ni Mamlaka za Udhhibiti, Tume ya Ushindani na Mamlaka ya kulinda haki na maslahi ya Watumiaji:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaunda mamlaka yenye nguvu ya kulinda haki na maslahi ya Watumiaji nchini;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga Sheria ya kuwalinda Watumiaji.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**438. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itaruhusu tena usafirishaji wa Vipepeo nje ya nchi ili kuongeza vipato vya Wananchi wa Muheza.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **439. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Uhamiaji katika Kijiji cha Chikongo kilichopo Kata ya Moreha Wilayani Tandahimba ambacho huduma ya VIZA kwa Watanzania waendao Msumbiji hutolewa.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
16 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**